

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA FEDHA NA UCHUMI



TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

BENKI YA MAENDELEO AFRIKA YATENGA DOLA BILIONI 5 KWA AJILI YA KILIMO

Hayo yamesemwa na Mkurugenzi wa Idara ya Kilimo wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB) Bw, Aly Abou-Sabaa alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari mjini Abidjan nchini Ivory Coast kwenye mkutano wa 45 wa Benki ya Maendeleo ya Afrika.

Bw. Abou-Sabaa aliendelea kusema kuwa kiasi hicho cha fedha kinatarajiwa kuelekezwa katika kusaidia miradi ya wakulima ili waweze kuwa na maeneo ambayo ni salama kwa ajili ya kuhifadha mazao yao mara baada ya mavuno ili yasiharibike na kuwaletea hasara ambayo ingeweza kuzuilika.

“Fedha hizi pia zitaelekezwa katika kuwasaidia wakulima kujenga mifumo ya maji ya umwagiliaji ili kuimarisha kilimo cha umwagiliaji kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa mazao mbalimbali.” Alisisitiza Abou-Sabaa.

Awali akitoa mada kuhusu mapinduzi ya kijani katika kilimo kwenye mkutano huo mtaalamu wa Sera wa Shirika linalojulikana kama “Alliance for Green Revolution in Africa” Dkt Augustine Langyintuo alisema kuwa hakuna nchi inayoweza kuendelea katika sekta ya

kilimo kama haitaweza kuongeza matumizi ya mbolea na hivyo kuongeza uzalishaji wa mazao.

Aliendelea kueleza kuwa iwapo nchi yoyote ikifanikiwa kuongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo kwa mwaka kwa wastani wa asilimia 10 itakuwa imepunguza hali ya umaskini kwa kiwango cha asilimia 4. Kwa sababu kilimo ni sekta pekee katika nchi za Afrika inayotoa ajira kubwa kwa watu, alisisitiza Langyintuo.

Langyintuo alisema kuwa ili kuwepo na matumizi mazuri ya mbolea ni vyema kodi ya mbolea ikaondolewa, gharama za kusafirisha mbolea kwenda kwa wakulina zikapunguzwa, kuondoa ;awakala wote ambao ni wazembe na kuwaweka ambao wanaweza kumudu kazi hiyo yakusambaza mbolea kwa wakulima wengi na hasa wadogowadogo.

Aidha Mkurugenzi huyo alimalizia kwa kusema kuwa sehemu ya fedha hizo pia zitaelekezwa katika kujenga mazingira mazuri kwa ajili ya wakulima ili waweze kuzalisha mazao yao kwa wingi.

Mikutano hii ya mwaka ya Benki ya Maendeleo ya Afrika bado inaendelea na inatarajiwa kufikia kilele chake hapo tarehe ishirini na nane mwezi wa tano mwaka huu.

Imetolewa na Msemaji Mkuu

Wizara ya Fedha na Uchumi

Abidjan

26.05.2010